# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI MAWASILIANO NA UCHUKUZI KWA MWAKA 2024/2025

***Mheshimiwa Spika,*** Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake kwa kunijaalia uzima na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza hili kuwasilisha hotuba ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

***Mheshimiwa Spika,*** Pili, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kwanza kuchangia hoja hii iliyopo mezani. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati tunachambua Fungu la Wizara hii pamoja na

wakati wote Kamati inapofanya kazi na Wizara hii.

Pia napenda kuwashukuru watendaji wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia Makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii.

***Mheshimiwa Spika,*** Pia naomba kutumia nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao makubwa wanayoendelea kunipatia ambayo yameiwezesha Kamati kufanya kazi kwa ufanisi na uweledi mkubwa. Kwa ruhusa yako sasa naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe hao pamoja na Makatibu wa Kamati kama ifuatavyo: -

| **Nam** | **JINA** | **WADHIFA** |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Yahya Rashid Abdalla | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe.  Aza Januari Joseph | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ameir Abdallah Ameir | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Hassan Hamad Omar | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Simai Mohammed Said | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 10. | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |
| 11. | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| 12. | Ndg. Saad Othman Saad | Katibu |

***Mheshimwa Spika,*** Kwa namna ya kipekee na udhati kabisa Kamati yetu inampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi na Serikali kwa ujumla kwa juhudi zake za kuongeza miradi ya Kimkakati ya Uwekezaji hasa miundombinu ya ujenzi wa barabara, bandari na viwanja vya ndege pamoja na mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawawakilishi Toleo la 2020, Kamati yetu imelichunguza na kulifikiria Fungu la Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuangalia utekelezaji wake kwa mwaka wa fedha unaomalizika na malengo waliyopangiwa kwa mwaka ujao kulingana na fedha walizopatiwa mwaka uliopita na wanazo omba kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wizara hapo mwakani.

## MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati imeridhika na mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha robo tatu kwa yale mapato yanayokusanywa na kuingia katika Mfuko wa Wizara hadi kuvuka lengo na kufikia asilimia 113.9. Pia Kamati imeridhishwa na makusanyo ya taasisi za Wizara hii zinazojitegemea ambazo nazo zimekusanya vizuri hadi kufikia wastani wa asilimia 75 hadi asilimia 166. Kamati inazipongeza taasisi hizo na inaziomba zisiridhike, na badala yake ziongeza kasi ya ukusanyaji ili ziweze kukusanya zaidi katika robo iliyobakia.

***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa upatikanaji wa fedha za matumizi kwa kazi za kawaida na Miradi ya Maendeleo, Kamati pia imeridhishwa na mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha katika bajeti ya Wizara hii hadi kufikia asilimia 75.

Hata hivyo, Kamati ilipochambua upatikanaji wa fedha kwa kila Programu tulibaini kwamba Programu ya Ujenzi na Majengo ya Serikali ilipatiwa asilimia 33 tu na Programu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nayo ilipatiwa asilimia 29 % tu za bajeti waliyoomba. Kamati haikuridhishwa na upatikanaji wa fedha kwa Programu hizo kwa sababu zimeathiri shughuli za kila siku pamoja na shabaha zilizowekwa na taasisi zinazotekeleza Programu hizo.

Kamati inaishauri Serikali kuweka kipaumbele cha kutoa fedha za matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa uwiano unaostahiki ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa kila siku wa Wizara na taasisi zake.

## UIMARISHAJI USAFIRI WA NCHI KAVU

### Barabara ya Wete- Chake

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeripoti kuendelea na ujenzi wa Barabara ya Wete- Chake inayotekelezwa na Kampuni ya MECCO ikiwa ni miongoni mwa Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu za Unguja na Pemba. Mradi wa Barabara ya Wete – Chake hadi kufikia mwezi wa Machi 2024 umefikia asilimia 25 tu za utekelezaji wakati kwa mujibu wa Mkataba kwa muda huo mkandarasi alitakiwa awe ameshafikia asilimia 78.6.

***Mheshimiwa Spika,*** Licha ya changamoto kadhaa zinazoelezwa na Mkandarasi pamoja na Wizara, Kamati haikuridhika kabisa kuhusiana na Maendeleo ya Mradi huu. Kwa kweli mradi unaendelea kusuasua na kukatisha tamaa. Kamati inaendelea kusikitishwa pamoja na kushangazwa na uvumilivu wa Serikali uliopo kwa wakandarasi ambao pamoja na kuaminiwa bado hawaoneshi uwezo na utayari wa kufanyakazi kama hii, na kwa ubora na wakati uliopangwa.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaiomba Serikali kufanya tathmini ya kina kuhusiana na uwezo wa wakandarasi kama hawa na baadae kufanya maamuzi magumu dhidi ya wakandarasi wa aina hiyo wanaopewa miradi kama hii ya kimkakati na kushindwa kwenda sambamba na kasi ya utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Nane.

Vile vile, Kamati inaendelea kushauri sehemu ndogo iliyokwisha kukamilika kwa kifusi iwekwe lami kama vile inavyoonekana katika barabara nyengine ili kuepusha hasara inayoweza kujitokeza kwa kifusi hicho kukaaa muda mrefu na barabara kuanza kuchimbika kabla ya utiaji wa lami kuanza.

***Ujenzi wa Barabara za Mjini pamoja na Barabara za Juu- (Fly over)***

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati kwa kiasi Fulani imeridhika na mwenendo wa Mradi huu na kama alivyoripoti Mheshimiwa Waziri mradi umefikia asilimia 69.62 kwa upande wa Barabara za Kawaida, na asilimia 21.54 kwa Barabara ya Juu (***Fly over***) ya Mwanakwerekwe. Kamati inasisitiza haja ya kuongeza kasi ya ujenzi na usimamizi wa Mradi huu ukizingatia asilimia 80 ya fedha zinazohitajika tayari zimeshapatikana.

***Ujenzi wa Barabara za Ndani Unguja na Pemba***

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati haikuridhika sana na utekelezaji wa Mradi wa Barabara za Ndani, kwani pamoja na kwamba unaendelea kutekelezwa kwa

upande wa Unguja na Pemba katika hatua tofauti lakini bado umefikia asilimia 41 tu za utekelezaji wake, sambamba na upatikanaji wa fedha za mradi huu ambao hadi kufikia Machi, 2024 fedha zilizopatikana ni asimilia 37 tu za makadirio. Tunaiomba Serikali kuingiza Fedha za mradi huu kama zilivyoombwa ili mradi huu uweze kukamilika kama ulivyotarajiwa.

***Matengenezo ya Kawaida ya Barabara***

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaishukuru sana Serikali kupitia Wakala wa Barabara Zanzibar kwa kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya Kawaida ya Barabara ikiwemo uzibaji wa mashimo kwenye barabara zilizojengwa kwa lami. Hatua hii inakwenda kutimiza moja ya jukumu la Wakala wa Barabara Zanzibar la kujenga, kutunza na kuzifanyia matengenezo barabara ili ziweze kupitika kwa usalama muda wote.

Hata hivyo, kwa masikitiko makubwa tunashuhudia baadhi ya barabara zetu zikiwa zimechakaa na zimejaa mashimo suala ambalo linaleta usumbufu kwa watumiaji wa barabara ikiwemo kuharibu vyombo vya moto, kusababisha ajali na kuongeza msongomano barabarani.

***Mheshimiwa Spika*****,** Kamati inaiomba serikali kukalimisha kwa haraka bajeti waliyoidhinishiwa kwa mwaka wa fedha unaomalizika pamoja na kuwaomba waheshimiwa wajumbe kuidhinisha fedha zote kama

zilivyoombwa kwa mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya Barabara zetu za Unguja na Pemba.

**Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani**

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia taasisi yake ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imeahidi kuimarisha usalama wa watumiaji wa barabara kwa kuwapatia elimu ya usalama barabarani makundi tafauti ya jamii pamoja na kufanya ukaguzi wa njiani ili kubaini wanaokiuka sheria, kanuni na miongozo ya usalama barabarani.  Kamati inaunga mkono azma hii ya Mamlaka na inaitakia kila la kheri utelekelezaji wa azma hiyo ambayo ni miongoni mwa jitihada za kujikinga na ajali zinazosababisha vifo na athari nyengine za kijamii na kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na azma hiyo njema ya Mamlaka bado kamati yetu inasononeshwa na hali ya Usimamizi wa Watumiaji wa Vyombo vya Moto hasa Madereva na wasaidizi wao (makonda), kutokana na tabia yao mbaya ya kujaza abiria na mizigo kinyume na walivyoruhusiwa. Aidha hali ya usafi na uvaaji wa sare kwa madereva na wasaidizi wao hivi sasa inaendelea kudorora.

***Mheshimiwa Spika***, Kamati pia hairidhiki na tabia ya baadhi ya madereva wa gari zinazochukua wanafunzi (School Bus), ambao huchukua wanafunzi

kupita kiasi hali ambayo sio tu inakwenda kinyume na utaratibu, lakini pia inatishia usalama wa watoto wetu.

Kamati pia inalalamikia tabia ya waendesha bodaboda juu ya vitendo vya ukosefu wa nidhamu ikiwemo mwendo kasi na kupakia abiria zaidi ya mmoja pamoja na tabia iliyojengeka katika jamii hivi sasa ya kuzigeuza bodaboda kuwa school bus. Kamati inalaani vitendo hivyo na kuiomba Mamlaka kuongeza usimamizi pamoja na elimu ya Usalama wa barabarani ili kuvitokomeza vitendo hivyo.

## UIMARISHAJI WA USAFIRI WA ANGA

***Mheshimiwa Spika,*** Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kusaini mkataba wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba. Kamati imejenga matumaini makubwa kwa uamuzi huu wa Serikali wa Kutekeleza Mradi huu wa kimkakati lengo likiwa ni kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na kuifungua Pemba kiuchumi. Hata hivyo, Kamati inaihimiza Serikali kukamilisha zoezi la ulipaji wa fidia linaloendelea hivi sasa kwa wananchi waliosalia ili ujenzi uweze kuendelea na kupunguza malalamiko kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati Mamlaka inajipanga kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama ili kukidhi viwango vya kimataifa kwa matengenezo ya

vifaa na mafunzo, Kamati inaisisitiza Mamlaka kuongeza usimamizi kwa watendaji wake hasa wanaohudumia abiria moja kwa moja kuwa na Mlahaka mzuri (*Customer Care*) kwa wanaowapatia huduma ili kuepusha malalamiko yanayoendelea kujitokeza hasa katika sehemu za upekuzi wa mizigo na abiria.

**Mheshimiwa Spika**, tukiwa bado katika eneo hili la Usafiri wa Anga, Kamati inaendelea kuishauri Wizara kuendelea kuzisimamia taasisi zote zinazotowa huduma katika viwanja vyetu vya ndege, pamoja na ukaguzi wa mara kwa mara wa vifaa na vyombo vya kusafiria ili kuhakikisha muda wote vinaendelea kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa vinavyoweza kutumika katika ajali, matukio pamoja na dharura za viwanja vya ndege (*airport emergences*) kwa mujibu wa taratibu na miongozi ya Sekta ya Anga Duniani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Serikali imepiga hatua nzuri sana katika Sekta ya Usafiri wa Anga kwa kuimarisha miundombinu ya Viwanja vya Ndege kuwa bora na vya kisasa Unguja na Pemba, pamoja na kuongeza Viwanja vya Ndege vidogo vidogo ndani ya Zanzibar, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mpango wa kufikiria kununua ndege ya Serikali itakayorahisisha shughuli za kiserikali hasa kwa viongozi wetu.

## Shirika la Meli

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuifanyia matengenezo makubwa Meli ya MV Mapinduzi II. Kamati yetu ilikagua matengenezo ya meli hiyo na kama inavyosomeka katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Matengenezo hayo hivi sasa yamefikia asilimia 80. Kwa kweli tunapongeza sana hatua iliyofikiwa hivi sasa.

Aidha, Kamati imefarajika na hatua ya Shirika ya kuanza kutekeleza Malengo yake yaliyojiwekea Mwaka jana ya ununuzi wa boti mbili ziendazo kwa kasi. Tunaliomba Shirika kuharakisha michakato ya ununuzi wa boti hizo ili ziweze kupunguza adha ya usafiri wa majini kati ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es Salaam.

## Shirika la Bandari,

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilisi imeridhika na Utendaji wa Shirika la Bandari kwa mwaka unaomalizika hasa katika kuhudumia vyombo, Mizigo na Makontena pamoja na kuimarisha Bandari zake za Mkoani, Mkokotoni na ujenzi wa bandari ya Shumba Mjini.

Kuhusu Bandari ya Wete, Kamati inalitaka Shirika la Bandari kumsimamia ipasavyo Mshauri Elekezi katika kukamilisha hatua zilizobakia baada ya upembuzi yakinifu ili kuendelea na hatua nyengine za ujenzi huo.

**Shirika la Mawasiliano (ZICTIA)**

***Mheshimiwa Spika,*** tukisoma mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato wa Shirika la Mawasiliano tunabaini kwamba yameongezeka kutoka asilimia 51.3 katika kipindi kama hiki mwaka jana na kuvuka lengo hadi kufikia asilimia 166 mwaka huu. Kamati ilipodadisi siri ya mafanikio haya ilibaini kwamba, ni mwamko wa wateja kulipia ada na tozo za huduma wanazopatiwa pamoja na ari ya wafanyakazi hasa baada ya mageuzi ya Taasisi yao kutoka Wakala na kuwa Shirika.

***Mheshimiwa Spika,*** Kwa Upande mwengine Kamati inalaani vikali vitendo vya uharibifu wa miundombini ya mkonga unaofanywa na watu binafsi pamoja na Taasisi mbali mbali, vitendo ambavyo vinalitia hasara Shirika na Serikali kwa ujumla. Tunaiomba Serikali kuchukua hatua kali kwa wale wote wanaoharibu miundombinu ya Shirika na kuisababishia hasara serikali. Aidha Kamati inaunga Mkono uanzishwaji wa huduma mpya ikiwemo Public WiFi.

**Wakala wa Majengo**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Majengo Zanzibar imo katika mchakato wa Kuandaa Sheria ya Wakala wa Majengo na tayari rasimu ya Sheria hiyo imekamilika. Kamati inaunga mkono hatua hii kwani itamuwezesha Wakala kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Kamati inahimiza uharakishwaji wa hatua zote za Sheria hiyo ili iweze kukamilika kwa wakati na hatimae kuanza kutumika.

***Mheshimiwa Spika,*** kwa kumalizia hotuba yangu Kamati inakubaliana na uwamuzi wa Wakala hapo mwakani wa kuandaa ramani na makisio ya gharama za ujenzi wa Nyumba za Viongozi pamoja na majengo mawili ya Serikali. Hatua hii itasaidia kuokoa fedha nyingi za Serikali zinazotumika kwa ajili ya kukodi nyumba za Viongozi na Ofisi za Serikali kwa baadhi ya taasisi.

***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mara nyengine tena napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha hotuba hii kwa niaba ya Kamati na pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuifatilia kwa ukaribu sana hotuba yangu hii na kwa kunisikiliza. Ni

matumaini yangu kuwa Wajumbe wataichangia, wataijadili na hatimae kuipitisha Bajeti ya Wizara hii kwani imebeba sekta muhimu sana za nchi yetu ambazo ndio mategemeo makubwa ya kuinua uchumi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** naunga Mkono Hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………….……………..

**(Mhe. Yahya Rashid Abdulla)**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**